**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,**

Sina budi kumshukuru Allah (S.W.T) mwingi warehma na utukufu, kwa kutujaalia uhai na Afya njema, na kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Tisa, kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ambao ndio sababu ya sisi kusimama katika Baraza hili. Aidha nakushukuru na kukupongeza wewe **Mheshimiwa Spika,** kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi na upeo mkubwa. Ni imani yangu kwamba, utaendelea kutuongoza kwa uadilifu na ustadi wa hali ya juu kwa lengo la kuimarisha Demokrasia katika chombo hiki muhimu cha kuwatumikia wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia,naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru na kumpongezakwa dhati Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote kwa jitihada kubwa wanazozichukua katika kulipeleka mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za Kamati, jambo ambalo limepelekea wepesi kwangu kuweza kuiongoza Kamati hii inayosimamia Wizara muhimu kabisa. Wajumbe wa Kamati wameonesha umahiri, weledi na umakini wa hali ya juu na wameweza kuijadili ipasavyo Bajeti hii na kuhoji mambo mengi ya msingi, kwa lengo la kuhakikisha fedha wanazoidhinisha katika Baraza hili, zinatumika vizuri na kwa lengo lakuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza na kuwashukuru Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu, kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi waliowachagua. Ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi hatuna budi kurejesha imani kwao, kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote, kwa dhamira ya kutetea maslahi yao katika Baraza hili tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, Naomba niwakumbushe wajumbe wenzangu kuwa kipindi chetu cha miaka mitano kinakimbia kwa kasi kubwa, hivyo kila mmoja wetu ajitahidi kutekeleza aliyoahidi na kwa pamoja tutakuwa tumemsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kukamilisha ahadi zake kwa wananchi waliotuchagua kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Kabla ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako, na kwa heshima ya kipekee naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kama ifuatavyo:

1. Mheshimiwa Yahya Rashid Abdallah — Mwenyekiti
2. Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis — M/Mwenyekiti
3. Mheshimiwa Abdalla Abbasi Wadi — Mjumbe
4. Mheshimiwa Bihindi Hamad Khamis — Mjumbe
5. Mheshimiwa Haji Omar Kheri — Mjumbe
6. Mheshimiwa Zawadi Amour Nassor — Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha Kamati hii inafanyakazi kwa kusaidiwa na Makatibu wawili ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kiasi kikubwa na kwa uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu, msaada wa makatibu hao umekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya Kamati hii. Makatibu hao ni:

1. Ndg. Fatma Omar Ali — Katibu
2. Ndg. Mussa Issa Mussa — Katibu
3. Ndg. Azmina Hamad Khamis — Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,**

Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya kila mwaka, hivyo katikakutekeleza jukumu hilo Kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, sasa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati, napenda kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha **2021/2022.**

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo, sasa naomba nitekeleze jukumu nililopewa na Kamati la kuwasilisha Maoni ya Kamati, mbele ya Baraza lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka huu wa fedha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imepangiwa kutekeleza Programu Kuu Sita (6) ambapo utekelezaji wake unasimamiwa na Programu Ndogo Tisa (9).

## PROGRAMU KUU YA ELIMU YA JUU

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo kuu la kuanzishwa programu hii ni kutoa elimu itakayomuwezesha kila muhitimu kujiari au kuajiriwa. Katika kuhakikisha utekelezaji bora wa programu hii kupitia programu ndogo iliopo chini yake huduma mbali mbali zinatekelezwa ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti, Huduma ya Sayansi na Teknolojia, Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini baadhi ya changamoto kadhaa katika kifungu **HK01030101**ambapo fedha zilizotengwa katika utekelezaji wa Huduma hii ya Chuo Kikuu cha SUZA haiendani na uhalisia wa utekelezaji wa shughuli za Chuo hicho. Hivyo, Kamati imewataka watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kukaa tena na watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili kufanyia marekebisho kifungu hicho.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati ilipokuwa ikipitia kifungu hiki fedha iliotengewa kwa Chuo hicho ni **Tshs. 2,384,000** ambapo fedha hiyo haitaweza kutekeleza azma na malengo waliojipangia hatimaye kutoa tija iliyokusudiwa ukilinganisha na fedha waliotengewa mwaka 2020/2021 ilikuwa jumla ya **Tshs.14,778,600 sawa na tofauti ya asilimia 16.3.**

**Mheshimiwa Spika,**

Changamoto nyengine iligunduliwa na Kamati ni kuzorota kwa utekelezaji wa Sheria Namba 7 ya Mwaka 2016. Sheria Ambayo ilifanya marekebisho ya kuzifuta baadhi ya Sheria na hatimaye kuviunganisha baadhi ya Vyuo vikiwemo Chuo cha Fedha cha Chwaka, Chuo cha Habari, Chuo cha Utalii na Chuo cha Afya kuwa chini ya utekelezaji na usimamizi ya SUZA.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inaiomba Serikali kuvirudisha Vyuo hivyo kama vilivyokuwa awali ili kuvirudishia hadhi na ufanisi wake kama ilivyo awali kwani Kamati imebaini kuwa kubakia Vyuo hivyo chini ya SUZA ni kuvidumaza na kuvipotezea fani zinazokusudiwa kupatikana.

Vile vile, Kamati inaiomba Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuipitia upya Sheria hiyo na hatimaye kuja na marekebisho katika Baraza hili ili kuweza kuendana na kasi ya awamu ya nane ya maendeleo kwa kuzalisha wataalamu waliobobea katika fani mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilipokutana na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imekumbana na kadhia ya ucheleweshwaji wa fedha za malipo kwa wanafunzi wetu waliopo Vyuoni. Hivyo,

Kamati inaiomba Wizara ya Fedha na Mipango kuwaingizia fedha kwa wakati Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili kuweza kuwapunguzia usumbufu wanafunzi wetu waliopo Vyuoni kwa kutolewa nje katika mitihani, kusimamishwa katikati ya Masomo (Semister) na mwengine hata kufukuzwa Vyuo kwa sababu tu ya kucheleweshwa kuingizwa kwa ada ya malipo ya Chuo husika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati haijaridhishwa na kuwepo kwa eneo dogo la Ofisi ya Bodi hii kwani jengo lao lina nafasi finyu na halijazingatia watu wenye mahitaji maalum (watu wenye ulemavu) hali inayompelekea Mkurugenzi kushuka chini pale inapotokezea mtu mwenye mahitaji maalum kafuata huduma katika ofisi zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mnasaba huu, Kamati inaiomba Serikali kwa Kushirikiana na Wizara ya Elimu kuharakisha Ujenzi wa Mradi wa Jengo Jipya la Wizara ambalo litajumuisha na taasisi zake zote zisizo na ofisi za uhakika,

## PROGRAMU KUU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa Programu Kuu hii Kamati itaizungumzia zaidi Programu Ndogo ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni **SK010402.**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imesikitishwa sana kwa kuona Serikali ya awamu ya Saba ya Mhe. Rais wetu Mstaafu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa nia njema na thabit ya kujenga Vyuo vya Amali viwili vipya kwa Unguja kilichopo Makunduchi na kwa Pemba kilichopo Daya Mtambwe ambapo hadi tunawasilisha taarifa hii kwenu Vyuo hivi vya Amali havijafanya kazi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Unguja Kituo cha Makunduchi Kamati hairidhishwi na vitendo vya Mkandarasi Aliyekabidhiwa Ujenzi huo wa Chuo hicho kwani hadi inatembelea eneo la Chuo hicho cha Amali kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya wa Kusini Ujenzi wa Chuo hicho kwa kiwango kikubwa umekuwa wakusuasua. Jambo lililopelekea Kamati kuhoji na kupitia mikataba ya Ujenzi huo na Kamati imebaini kuwa Mkataba wa Ujenzi ushamaliza muda wake tangu mwaka 2016 pamoja na kuongezewa muda Mkandarasi huyo kwa zaidi ya mara mbili bado Mkandarasi hadi sasa hajakamilisha baadhi ya kazi za ndani zilizobakia hali iliyosababisha watoto kushindwa kujiunga na mafunzo kwa mwaka huu wa fedha ambapo kwa mujibu wa taarifa tulizopokea kutoka Wizara husika Chuo hicho kilitakiwa kuanza kusomesha mwezi wa Februari mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,**

Chakushangaza Mkandarasi huyo anatumia fedha anazolipwana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza ujenzi wa miradi Mengine aliyoingia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana.

**Mheshimiwa Spika.**

Hivyo, Kamati inapendekeza kwa Serikali na Wizara husika mradi huu kufuatiliwa kwa kina utekelezaji wake na kuiomba Taasisi ya Kupambana na Ruchwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) kuufanyia kazi Mradi huu kwani umekuwa na hitilafu nyingi za kiutekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, Kamati inaishauri Serikali katika Miradi ya Ujenzi ya Maendeleo kuwashirikisha kikamilifu wataalamu wetu wa ndani wa Wakala wa Majengo wa Serikali (ZBA) mapema

ili kuweza kumfuatilia Mkandarasi anayekusudia kukabidhiwa kazi kutathmini utendaji wake kabla ya kupewa mkataba wa kazi kwani Kamati imebaini baadhi ya Wakandarasi wanaokabidhiwa kazi hawana viwango na uwezo wa kufanya kazi. Mfano halisi ni Mkandarasi huyu mwenye kufika mpaka kuwakopa fedha wananchi wa kijiji cha Makunduchi ili kuendeleza kazi zilizobakia katika mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Pemba Ujenzi wa Mradi huu umekamilika na baadhi ya vifaa tayari vipo sababu iliyopelekea kushindwa wanafunzi kuanza masomo ni kukosekana na walimu wenye taaluma zinazotakiwa kutolewa pamoja ukosefu wa fedha za ununuzi wa vifaa vya kusomeshea kwa vitendo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati iliwaomba wahusika kwenda kwa Katibu Mkuu Kiongozi kuelezea mahitaji yao na umuhimu wa kupatiwa nafasi za ajira za wataalamu hao katika kada tofauti ili Chuo hicho kiweze kuanza masomo kwa wanafunzi kama lengo la Serikali yetu sikivu ilivyojipangia kwani kuchelewa kuanza masomo ni kuwakosesha haki ya Elimu watoto na kuwavunja moyo na kukatisha matumaini kwa wale watoto waliokuwa tayari washajisajili.

## PROGRAMU KUU YA UBORA WA ELIMU

**Mheshimiwa Spika,**

Dhumuni kuu la programu hii ni kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu kwa Unguja na Pemba. Huduma zinazotolewa kupitia Programu ndogo iliopo chini yake ni pamoja na Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia, Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu, Huduma ya Ukaguzi wa Elimu, Huduma ya Maktaba, Huduma ya Urajisi wa

Elimu, Huduma ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha na Huduma ya kuibua Vipaji vya Michenzo vya Wanafunzi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati katika kufanya kazi zake za kupitia bajeti ya Wizara hii imebaini na kushangazwa na fedha kidogo iliyotengwa mwaka huu wa fedha 2021/2022 kwa Kifungu cha **HK01050106**ni **Tshs. 100,000,000**ukilinganisha na mahitaji yanayotumika hususan kwa watoto wenye mahitaji maalum kwani kama tunavyojua vifaa na mahitaji yao huwa ya gharama kubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Sambamba na hilo, Kamati imesikitishwa sana kwa kuona kwa mwaka wa fedha 2020/2021 huduma hii ilipangiwa fedha **Tshs. 575,127,500** kwa kazi za kawaida ambapo hadi kufikia Aprili, 2021 fedha zilizopatikana ni **Tshs. 16,020,000** tu sawa na asilimia 3 ya utekelezji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na kadhia hii, Kamati inaiomba Serikali pamoja na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuliangalia tena fungu hili kwani kukosekana kwa fedha na kutengwa kwa fedha ndogo kwa kutekeleza huduma hii kunapelekea watu wenye mahitaji maalum kukosa huduma muhimu hususan katika sekta ya Elimu.

**Mheshimiwa Spika,**

Licha ya Ukwasi wa fedha wanaoupata Idara/Wizara hii, Kamati inapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza watendaji wote wa Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kwa kukamilisha kwa wakati Sera ya Elimu Mjumuisho kwani kuwepo kwa Sera hiyo itatoa mwaga na miongozo katika Sekta ya Elimu Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu kifungu **HK01050103** Kamati haikuridhishwa na madeni ya ndani waliyoyakuta ya **Tshs. 31,000,000** Milioni yatokanayo na kazi za kawaida ikiwemo za ukaguzi ambapo lalamiko kubwa limeonekana madeni hayo yanatokana na kukosekana au kuchelewa kupatikana kwa wakati kwa fedha iliyotengwa kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,**

Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kulitafutia ufumbuzi suala zima la ucheleweshwaji wa uingizwaji wa OC za matumizi mengineyo za Wizara pamoja na Taasisi zake kwa wakati na kama zinavyoidhinishwa na Muhimili huu wa Nchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, Kamati haikufurahishwa na utekelezaji wa Bodi ya Ukaguzi wa Elimu ambapo tangu kuanza kwake katika vikao vyao vyote walivyofanya hata siku moja haikuwahi kushuka chini katika gazi ya utendaji wa wakaguzi wake wa Elimu angalau kuzungumza nao pamoja na kuwasikiliza changamoto wanazokumbana nazo katika kutekeleza jukumu hilo kwa Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, Kamati imebaini kupitia Ofisi hii kuwa hadi tunawasilisha taarifa hii ndani ya Baraza lako Tukufu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haina Muongozo wowote unaohusiana na Viwango vya Upatikanaji wa Walimu walio Bora *(Teacher's Standard Proffessional)* hali inayopelekea watoto wengi kutofaulu katika masomo yao katika gazi

tofauti za Elimu ikiwemo Msingi, Sekondari hadi Vyuoni pamoja na kuajiri Walimu wasiokuwa na Viwango.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuharakisha uaandaji wa Muongozo wa Viwango vya Walimu ili kuweza kuondokana na kadhia ya ufaulu mdogo wa watoto wetu pamoja na kuondokana na uajiri wa walimu wasio na maadili na sifa za Ualimu.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ELIMU

**Mheshimiwa Spika,**

Utekelezaji wa Programu Kuu hii unatekelezwa kupitia programu ndogo tatu (3) ikiwe Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Programu ya Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti za Wizara na Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Wizara Pemba.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPNGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kukamilisha Sera ya Elimu ya Msingi na Sekondari kwa wakati. Aidha, Kamati inaiomba Idara hii kusimamia na kupanga vyema kazi za Wizara kwani Kamati imeona kuwa Wizara hii inakumbwa na changamoto nyingi haswa katika utekelezaji na usimamiaji wa Miradi Mikubwa ya Ujenzi wa Maendeleo katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba mwisho wake kupelekea upotevu wa Fedha na Rasilimali za Serikali.

## PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia imegundua kuwepo kwa changamoto ya uhaba wa walimu wataalamu wa Sayansi, madeni makubwa ya nauli za walimu pamoja na maposho yao ya (Over time) kuchelewa kupatikana kwa wakati hali inayowawia vigumu walimu wetu kufanya kazi vizuri na katika mazingira magumu ya kiutendaji.

**Hitimisho**

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena, wewe binafsi, **Mheshimwa Spika**, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni kwa niaba ya Kamati yangu, pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa, sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii, ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka huu wa Fedha unaokuja.

**Mheshimiwa Spika,**

Mimi mwenyewe binafsi nakwa niaba ya Kamati ninayoiongoza ya Ustawi wa Jamii, naiunga mkono hoja kwa asilimia 100%.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya Maelezo hayo, **naomba kuwasilisha.**

**Ahsante,**

……………………………
Mhe. Yahya Rashid Abdallah,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**